

URITHI WETU:UWANA

“Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo; na ndani yake sisi tulifanywa urithi, hukutukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake” (Waefeso 1:10-11).

“Urithi.” Tumepata urithi. Mtu fulani hana budi kukuachia kitu fulani. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuachia kitu fulani. Jina lilioandikwa katika Kitabu, ili kwamba Mwana-Kondoo akichinjwa utatambulikana pamoja Naye.(Ufunuo 13:8)

“Na ndani yake sisi nasi tumepata urithi”, Tunapataje urithi huu hapa? Kwa kuwa tulitembea imara? Tunaupataje urithi huu? Kwa kuwa tulichaguliwa tangu zamani.

Mnaona, urithi. Ni urithi wa namna gani? *“...huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.”*

Kabla Yeye hajawa Baba, kabla hajawa Mungu, kabla hajawa Mwokozi, kabla hajawa Mponya, kabla ya mambo haya yote, yeye alitangulia kuchagua, akaliandika Jina la Mwana-Kondoo katika Kitabu, akaangalia chini kwa kujua Kwake tangu awali na kuliona jina lako, akaliandika mle pia. Ni kitu gani? Na baada ya kitambo kidogo tukaja ulimwenguni, tumezaliwa na wazazi wenye dhambi(Warumi 3:23-24; Zaburi 51:5); tunatembea kila mahali ulimwenguni.

Akatuchagua tangu zamani kwa ajili ya urithi wetu katika Yeye, uliochaguliwa tangu zamani kwa ajili yetu; tuliurithi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kwa ajili ya kusudi Lake Mwenyewe kutekeleza mapenzi Yake mema, hiyo ni kweli kabisa, kuwa Mungu na Mwokozi.

Kurithi kwa kuchaguliwa tangu zamani. Mimi nilirithi kitu fulani. Urithi gani? Ilipaswa kuwepo na mtu fulani aniachie urithi. Mbona, unasema, “Yesu alikuachia urithi.” Ati nini? Yesu hakuniachia urithi, Yesu hakukuachia urithi; Yeye alishuka tu akaja akalipia urithi wako, akakuleta kwenye urithi wako. Bali jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu ndiye aliyekupa urithi wako. Urithi wako ndio uliokuja kwanza. [1]

Loo, “urithi.” Mtu fulani hana budi kukuachia kitu fulani, kukirithi. Sivyo? Urithi! Tuna urithi gani? Mimi nilikuwa na urithi gani? Sikuwa na wo wote. Bali Mungu aliniachia urithi alipoandika jina langu katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.(Ufunuo 13:8, Ufunuo 17:8) Loo, unasema, “Sasa, ngoja kidogo, ndugu, Yesu alifanya hivyo alipokufa kwa ajili yako.” La, hakufanya hivyo. Yesu alikuja kununua huo urithi kwa ajili yangu.

Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kama jinsi tulivyoona kwamba Mungu aliishi peke Yake, jinsi ambavyo katika Yeye.mlikuwemo na upendo. Katika Yeye mlikuwemo kuwa Mungu; hapakuweko na kitu cha kumwabudu. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Baba; kulikuwa...Yeye alikuwa peke Yake. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Mwokozi; hapakuwepo na kilichopotea. Ndani Yake mlikuwemo kuwa Mponya. Hizo ni sifa Zake. Hapakuwepo na kitu hapo. Kwa hivyo Yeye Mwenyewe, shauri la mapenzi Yake Mwenyewe lilitoa mambo haya, ili kwamba katika Mtu huyu mmoja, Kristo Yesu, avikusanye vitu vyote pamoja tena. Loo! “Jicho halijaona, sikio halijasikia...”(1Wakorintho 2:9-10) Si ajabu ni jambo la ajabu!

Tazama, “ametuchagua tangu awali tupate huu urithi.” Kama mimi nina haki ya kurithi kitu fulani, kama Mungu anabisha moyoni mwangu na kusema, “Nalikuwa wewe muda mrefu uliopita, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuihubiri Injili,” nina urithi, urithi wa Uzima wa Milele. Sasa, Mungu alimtuma Yesu kuufanya urithi huo halisi kwangu, kwa kuwa hakuna kitu ningaliweza kufanya ku—kuurithi. Ulikuwa mtupu, ulikuwa halali, nisingeweza kufanya lo lote. Bali katika utimilifu wa wakati Mungu alimtuma, katika wakati Wake uliofaa, Yesu aliye Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu(Wagalatia 4:1-7). Damu Yake ilimwagika kusudi nipate kwenda kwenye urithi wangu(Wakolosai 1:12-15; Waefeso 1:7). Kuwa nini, urithi gani? Uana, kuwa mwana wa Mungu.

Tulipewa urithi vipi, kwa njia gani? Kuchaguliwa tangu awali. Kuchaguliwa tangu awali ni kujua tangu zamani. Mungu alijuaje kwamba angekuaminisha kuwa mhubiri? Kujua kwake tangu zamani. “Si kwa uweza wa yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, Ni Mungu mwenye kurehemu.”(Warumi 9:14-16) Hiyo ni kweli, kuchagua tangu awali. Yeye alijua kilichokuwa ndani yako. Alijua kilichokuwa ndani yako kabla hata hujaja duniani. Alijua kilichokuwa ndani yako kabla hapajakuweko na dunia ambamo ungeishi. Huyu ni Yeye. Huyu ni Mungu asiye na kikomo, yule asiye na kikomo. Sisi tuna kikomo, tunaweza tu kuwazia yaliyo na kikomo. [2]

Sasa,tuna Amana takatifu.Mnajua ni amana gani. Na tuna Urithi, Urithi ambao tumerithi, kama watoto wanaoamini. Ni amana takatifu. Na hiyo amana takatifu na urithi mtakatifu ni Neno la Mungu ambalo tumepewa, Neno kamilifu la Mungu. Neno lenyewe ni kirutubisho, Neno lenyewe, Neno la Mungu!

Hapo ndio, sababu mimi ni Imara, kama jinsi nilivyoliita,kusimama katika hili neno! Haidhuru chochote kile kingesema, kama hakiko pamoja na neno,sitaamini hilo;unaona, unataka kuamini hilo, Hiyo ni sawa. Lakini kwangu,huchukua Neno, sababu, “Mbingu na nchi zitapita, Ila maneno yangu hayashindwa kamwe”(Mt Mathayo 24:35). Hivyo basi, huchukua(Hubidi) hilo Neno!

Ninaishi kwa Neno. Yesu alisema, “Imeandikwa Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu”(Mathayo 4:4). Na hivi ndivyo! Na hilo limetolewa kwetu kama urithi. Ni urithi wetu, Neno!

Ee Mungu, hebu na tufanye kuwazia hilo kwa kina.

Ni upendeleo wetu. Ni hii Amana takatifu ambayo Mungu ameweka kwa kanisa lake. Mungu ametoa Neno lake kwa kanisa lake. Na ule urithi mtakatifu ni wetu. Ni Zawadi kutoka kwa Mungu. Sio kulalamika

juu ya hili,na kuondolea hili mbali, na kutupilia hili nje, na kuongeza hili ndani ya hilo, kupendezesha ladha yetu; bali kuhubiri Neno kamilifu, Injili yote. Tunawajibika, kama Wakristo, Kuchukua Hilo na kuliadini. Tunapofahamu, “Kama Mioyo yetu isipotuhukumu, basi twajua tuna upendeleo kwa Mungu”(1 Yohana 3:21-22).

Ni juu yetu, ambao Neno limeletwa kwetu.Ni juu yetu, kwamba tudumu na hilo Neno. Na kadri tutavyodumu nalo, tutamuona Mungu akitenda miongoni mwetu. Hivyo inakua juu yetu, kudumu na hilo.Ni urithi ambao Mungu ametupa sisi.

Hicho ndicho tunachorithi, ni Neno.Na katika wakati mgumu,katika wakati wa dhiki,katika wakati wa kufadhaika,katika wakati wa hatari wanapata faraja kwa kushikilia Neno.

Neno ni faraja ya Mungu.Wakati unapojua, na unaweza kutembea hata katika bonde la uvuli wa mauti,na unajua kwamba Mungu amesema hivyo,hiyo hutuliza hilo. Mungu amesema!(Zaburi 23:4). [3]

Kama utapata urithi ulimwenguni hapa, rafiki, ni urithi unaoharibika.Lakini tunapokea urithi usioifia kamwe. Mwana mpotevu alikwenda mbali na kuacha urithi wake, na kuchukua sehemu ya huo urithi pamoja naye(Luka 15:11-32). Aliporejea ,urithi wake ulikua umenajisiwa. Lakini unapokimbia kutoka katika urithi wako, Sio hivyo katika ufalme wa Mungu;Tunapokea urithi usioharibika. Je hungenda kupokea huo?

Pengine walirithi kiasi Fulani cha pesa kutoka kwa mtu Fulani wakati mmoja, lakini hizo zingefanya nin? Hawakujua hata zilikwenda wapi,iliisha tu baada ya kitambo Fulani, sababu ilikua urithi uharibikao. Na kama wangeuacha kwa mtu mwingine, ungeharibika tena.

Lakini tuna Urithi usioharibika; huo ni wokovu, ukombozi, rudi nyuma tena Bustani ya Edeni(1Petro 1:3-4) Wazia kuhusu hilo, Bwana,Nani asingetamani kurudi kama Adamu na Hawa na kuishi pale, tukipewa chakula chetu kila siku; Baba wa Mbinguni kila siku akizungumza nasi; kuona ule mwangaza mkuu ukitembea mbele yetu. Simba na mbwa mwitu wakila pamoja,Ng’ombe akila majani, Simba akila pamoja naye; ila sasa wanakulana mmoja kwa mwingine, ama samba humla Ng’ombe,na mbwa mwitu anamla ng’ombe, chochote angeweza kula. Lakini katika siku zao haikua hivyo. Ndege wakubwa wazuri wakiruka. Hakutakua na huzuni. Hakutakua na alama kamwe kwamba tumepita tumainiletu. Chini kule njiani tunawaona watoto wetu na wapendwa wetu. Ee Mungu, ni siku ya namna gani, Siku ya jinsi gani! Haijalishi kile tumepokea hapa duniani, Vyote tuvatkwenda kutoweka, Lakini huo hautafifia kamwe. [4]

Tunarithi kitu gani? Uzima wa milele. [2]

„ Yeye asikiaye maneno yangu,na kumuamini aliyenipeleka, yuna uzima wamilele, wala haingii hukumuni; bali amepita kutokamautini kuingia uzimani.” (Yohana 5,24).

Lakini, “Yeye atambuaye, yeye anayejua mahali pake katika wakati huu, yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna” (wakati wa sasa) “Uzima wa Milele. Hataingia Hukumuni, bali tayari amepita toka mautini akaingia Uzimani.” Ndipo wakati Uzima huu mpya wa Milele unapokaa ndani yako, Hiyo ni dhamana, ama ni arabuni ya wewe kuhuishwa kutoka katika mwili huu ulio katika hali ya kufa kuingia katika mwili usiopatikana na mauti.

Hebu niliseme jambo hilo tena. Wakati Roho Huyu amekupata, wewe mtu binafsi, na amekuja juu yako, Yeye ni dhamana ya urithi wako wa Milele ambao Mungu alikuwazia na kukufanyia kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni arbuni yako.(Waefeso 1:13-14).

Ni kama vile ambavyo ungeniomba nikupe mwaloni, na nikupe mbegu ya mwaloni. Sasa, maisha ya mwaloni yako ndani ya mbegu ya mwaloni sasa, bali inakubidi kungoja mpaka itakapokua.

Vivyo hivyo na sisi. Unapompokea Roho Mtakatifu wa Mungu, ni uwezekano wa Mungu unaokungojea, ambao umekutambua tayari. Nawe umetiwa muhuri na Roho wa ahadi, wa Mungu, ukaingizwa katika Mwili wa Kristo(1 Wakorintho12:13). Wakati Mungu alipoangalia chini pale Kalvari na kumwona Yesu akifa. Alikufa kwa ajili ya Bibi-arusi Wake, ule Mwili, ambao ni Kanisa Neno, Kanisa linaloamini Neno la Mungu la wakati huo. Kristo alikuwa akitokwa na damu na anakufa. Na Mungu, alipokuwa akimwangalia, aliona ufufuo Wake, nalo Kanisa lilifufuka pamoja Naye wakati wa Pasaka (Waefeso 2:4-7).

Sasa angalieni. Ni arbuni, au ni uwezekano, zile nguvu za kuhuisha za kufufuka kwako, wakati unapompokea Roho Mtakatifu. Sasa anakaa ndani yako, ule uwezekano wake(Warumi 8:22-23).

Angalia, sasa uko safarini, ukikua kufikia ufufuo mkamilifu. Hakuna mti unaokua kwa usiku mmoja. Hauna budi kukua, kama tunavyokua katika neema na maarifa ya Mungu...(2Petro 3:18) Unabatizwa katika Roho Mtakatifu.Linanza kukua. Matawi ambayo yamekufa,yapogoe tu hayo; Bali Mti huo ungali unakua, ungali unaendelea, kwa sababu hauna budi kufikia ule ufufuo.

Wao wanaongozwa na Roho, kulihuisha Neno kwenu ninyi ambao ni waaminio(Warumi 8:14). Neno linaendelea kuhuisha, unapofikia kwenye tawi la kwanza, tawi la pili, tawi la tatu, na kuendelea kwenda juu. Anaendelea tu kuhuisha. Roho wa Mungu anaendelea kuhuisha kwako.Angalia jambo hilo, Pentekoste, miili yao ilihuishwa na Uzima mpya walioupokea. [5]

Nukuu:

[1] “Kufanywa wana wenye Mamlaka sehemu ya 3”(60-0522M), Aya 170-174,177

[2] “Kufanywa wana wenye Mamlaka sehemu ya 4”(60-0522E), Aya 72-75,89,102

[3] “Mfariji” (61-1001E), Aya 52-55,62-64

[4] “Ufunuo sura ya 5 sehemu ya 2”(61-0618), Aya 240-243

[5] “Muhuri ya Pasaka”(65-0410), Aya 92-100

Jiwe la kiroho la kujengea na. 10 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Joseph C Kanju

Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: kanjujoseph23@gmail.com
Cellphone: 0654335361